# USALITI WA KUAMIANA

MARCO SHIGELE MAPEMBE

Kitabu hiki
kimeandikwa na;Marco
Shigele Mapembe.

Namba za simu: +255743911993/
+255789059889

Barua pepe:

marcoshigele@gmail.com

Kahama – Tanzania

Kimechapishwa na BFI PUBLICATIONS

P. O.BOX 2942

DAR ES SALAAM – TANZANIA

© Marco Shigele Mapembe 2023

ISBN: 978 - 9987 - 12 - 046 - 8

Haki zote zimehifadhiwa © 2023. Huruhusiwi kunakili, kudurufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki pasipo na idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa kitabu hiki. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi, na ukiukwaji wa taratibu. Ni kosa kisheria.

# YALIYOMO

SHUKRANI………………… iii

UTANGULIZI .............................. iv

**SURA YA KWANZA**

USALITI, USALITI, USALITI... 1

**SURA YA PILI**

USALITI KATIKA MAENEO YA KAZI……4

**SURA YA TATU**

USALITI KATIKA UHUSIANO WA KIMAPENZI AU NDOA………25

**SURA YA NNE**

USALITI KATIKA BIASHARA… ......33

**SURA YA TANO**

KUSALITIWA NA NDUGU… ..........45

**SURA YA SITA**

TAHADHARI JUU YA USALITI ......53

MADHARA YA USALITI ................ 55

NAMNA YA KUPONA KUTOKA KWENYE USALITI… ......................57

NUKUU ZA KITABU… ......................58

# SHUKRANI

Awali ya yote namshukuru sana Mungu kwa kunipa neema na kibali cha kuandaa kitabu hiki chenye kubeba maudhui na mafundisho yatakayoisaidia jamii kwa ujumla. Lakini pia nawashukuru sana wazazi wangu na familia yangu kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kukamilisha kazi hii.

Na pia niwashukuru watu wote waliohusika kwa namna moja au nyingine kunisaidia kimawazo, ushauri na maombi katika kuandika kitabu hiki. Haikuwa rahisi kuandaa kazi hii lakini kwa mchango mkubwa wa kampuni ya BFI PUBLICATIONS kazi hii imefanyika kwa wepesi na weledi wa hali ya juu.

Asante.
Marco Shigele Mapembe

# UTANGULIZI

USALITI WA KUAMINIANA; Hiki ni kitabu pekee kinachoelezea swala zima la usaliti katika jamii, usaliti katika kazi, mahusiano ya kimapenzi/ndoa, kibiashara na kifamilia. Kitabu hiki kina hadithi za kusisimua zinazosaidia kufundisha jamii ni kwa namna gani usaliti unavyoleta madhara makubwa katika jamii, ndani ya nyanja chache muhimu za maisha yaani kazini, mahusiano au ndoa, biashara na kifamilia.

Vilevile kitabu hiki ni tiba kwa wale waliosalitiwa katika maeneo tofauti, kwani kitawasaidia kuepukana na usaliti kwa mara ya pili na pia kupona kabisa na maumivu au madhara waliopata baada ya usaliti.

Mwisho kitabu hiki kimebeba mafundisho makubwa ambayo yatamsaidia msomaji kuishi vizuri na kupata mafanikio makubwa katika maeneo ya kazini, mahusiano au ndoa, biashara na familia kwa ujumla.

# SURA YA KWANZA

## ===USALITI, USALITI, USALITI ===

## ====SEHEMU YA KWANZA ====

Dunia hii haina huruma, mtu yuko tayari kufanya chochote kwa mwenzie kwa faida yake mwenyewe. Mtu anaweza kujivunia kuharibu maisha ya mtu mwingine. Anafanya jambo bila hata kujali kuwa kitatokea nini kwa mwenzie. Mtu yuko tayari kufanya kitendo cha kinyama kwa mtu ili yeye ajinufaishe kwa namna moja au nyingine. Ndugu anaweza kumsaliti ndugu yake kwa kufanyiwa hata ukatili wa kijinsia kwa sababu ya vipande vya fedha. Dunia hii kweli imeharibika sana. Rafiki yuko tayari kumsababishia rafiki yake matatizo kazini ili yeye achukue madaraka. Mfanyabiashara yuko tayari kumsaliti mfanyabiashara mwenzie na kusababisha hasara. Mtu yuko tayari kumsaliti mke au mchumba wake kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke mwingine bila kujali maumivu atakayoyapata mwenzie.

Usaliti ni hatari kwa maisha ya mwanadamu. Unaweza kusababisha madhara makubwa sana. Kuna watu wanafanya hayo kwa sababu ya tamaa ya vitu au mali. Tamaa ya madaraka, vile vile ni chanzo cha usaliti. Watu wengine wanawasaliti wenza wao kwa sababu ya tamaa za mwili. Hebu, tujaribu kujiuza maswali yafuatayo:

Mbona furaha yao inaumiza wenzao?

Wanajisikiaje mtu anapolia kwa sababu

yao?Je, maumivu ya usaliti wanaweza

kuyabeba?

Je, wanaweza kulipa gharama ya maumivu yausaliti?

Je, hawajui kwamba usaliti unaweza kusababishakifo?

Kwa nini wanachezea hisia za watu?

Kwa nini wanapoteza IMANI ya watu kwa watu?

======SEHEMU YA PILI ======

Mtu anaweza kusalitiwa kwa siri kuvuja.

Anaweza kusalitiwa kazini, katika mahusiano, biashara na kwa ndugu.

Maswali ya kujiuliza kwa wasaliti:

Kwa nini watu wanaisaliti imani kwa maana ya **Trust**?

Je, hawajui kwamba, watu wanapowaambia mambo yao maana yake wamewaamini?

Mbona wanashindwa kuwa waaminifu? Mateso anayoyapata mtu kwa sababu ya kushushwa cheo au kufukuzwa kazi wao wanayafurahia? Wanajisikiaje kuvunja mahusiano au ndoa ya jamaaa zao?
Je, wanafurahi kuharibu biashara za watu?
Je, wanafurahi watoto wa watu kulia kwa sababu ya njaa kwa kuharibu maisha ya watu?
Kwa nini wanakuwa sehemu ya uharibifu?

# SURA YA PILI

## =USALITI KATIKA MAENEO YA KAZI =

## =====SEHEMU YA KWANZA =====

Sasa tusome usaliti unaotokea kazini.

Katika mahala pa kazi, kitu kikubwa kinachofanywa na wasaliti, ni kushambulia kitu kinaitwa "**Trust**". Yaani wanaishambulia "Imani" iliyopo aidha kwa Boss wako,au Kwa wafanyakazi wenzio na kuonekana mtu wa hovyo kabisa. Mashambulizi hayo, hufanywa na rafiki zako uliyokuwa unawapa siri zako. Walijifanya kuvaa ngozi ya kondoo kumbe ndani ni chui. Wanafanya hivyo aidha kwa maslahi yao ya moja kwa moja au kwa kutumiwa na watu wengine. Ooh! siri zako zinakuangamiza mwenyewe.

Kuna usemi wa lugha ya Kiingereza unasema "Your Best Friend Can Be Your Worst Enemy".

Yaani kwa tafsiri isiyo rasmi ni kuwa, " Rafiki yako wa karibu anaweza kuwa adui yako mkubwa".

Kumbuka ya kuwa, rafiki anaaminiwa na kutumainiwa. Lakini sasa, anaweza kugeuka na kuwa mbwa mwitu kabisa.

Rafiki yako, anaweza kujipendekeza kwa boss mara kwa mara, huku akikuharibia mambo yako, ili yeye aonekane bora zaidi kuliko wewe.

Oooh! marafiki siyo wa kuuwamini kabisa, kwa kifupiusimwamini kila mtu.

Swali la kujiuliza:

Kwa nini wanayafanya mambo hayo?

Jibu ni rahisi sana: Kama wewe ni Boss, na wao wanataka U-boss.

Kwa lugha nyingine wanasumbuliwa na tamaa ya madaraka.

Kwa mfanyakazi wa kawaida, wanataka tu mambo yako yaharibike ili wafurahi. Yawezekana ni wivu tu.

Maswali kwa msaliti:

Lakini sasa, kama wewe umepata madaraka kwa kumsaliti mwenzio, je, unayo amani ya moyo kukikalia kiti hicho ulichokipata kwa fitina na udhalim Je, hujui kwamba kuna watu wanalia kwa sababu ya wewe kukalia kiti hicho?

Ndugu, kumbuka Mungu yupo!!!

Unaweza **kupigwa kalamu** wakati wowote na **ukakata kamba** kwa sababu ya laana na madhara yaliyosababishwa na usaliti.

Unaweza kujipa moyo kwa kusema "**Dua lakuku halimpati mwewe**".

===== SEHEMU YA PILI =====

Tunaendelea na kipengele cha usaliti katika eneo lakazi.

Ngoja tuangalie kisa kimoja cha Mr. Chavek ambaye alikuwa ameajiriwa kama Mkurugenzi kwenye kampuni ya kuchakata vitu vya plastiki na kuwamafuta ya dizeli.

Bwana Chavek alikuwa na msaidizi wake ofisiniaitwaye Mr. Maliket.

Mr. Maliket alikuwa na cheo cha Naibu

mkurugenzi. Naibu mkurugenzi alionekana mwema sanamachoni pa watu.

Mr. Chavek alimwamini sana Naibu mkurugenzi wake kiasi kwamba akawa anamshirikisha mambo yake ya kifamilia na mipango yake ya baadaye.

Watu hawa walifanya kazi kwa pamoja na kwaupendo mkubwa sana.

Kadri siku zilivyokuwa zinaenda mbele, ndivyo Mr. Maliket alivyokuwa anatamani kuwa Mkurugenzi wakampuni.

Figisu zikaanza kwa boss (ambaye ni mmiliki wa kampuni), mara ooh, Mr. Chavek ana mambo mengina wala hana mpango wa kukaa muda mrefu katika kampuni hii kwa sababu ya. yaani akatoa siri zote,
zikiwemo changamoto za familia yake na mipango yake ya baadaye.

Boss, ambaye alijulikana kwa jina la Mr. Benok, akatafakari kwa kina sana na kuona kwamba Mr. Chavek hana **future** na kampuni.

Kwa hiyo akachukua maamuzi ya kumshauri ajihudhuru nafasi yake kwa maslahi mapana ya kampuni.

Hatujui, Mr. Maliket alitia chumvi gani kwa bossmpaka boss akafikia maamuzi hayo.

Mr. Chavek hakuwa na namna nyingine ya maamuzi tofauti na kuridhia maamuzi ya Boss.

Mr. Chavek aliandika barua ya kujihudhuru wazifa wake kulingana na maelekezo ya bosi na kazi ikaishia hapo.

Siku chache baadaye, Mr. Maliket alipandishwa cheo na kuwa mkurugenzi wa kampuni.

Baada ya kujihudhuru wazifa wake, Mr. Chavek aliandamwa na changamoto mbalimbali.

Watoto wake wawili waliokuwa wanasoma chuo kikuu kwa kuwalipia ada na michango mingine yeye mwenyewe, walishindwa kuendelea na masomo ya chuo.

Mke wake, aliyejulikana kwa jina la Kreso, akawa anamsumbua kwa kumuomba fedha za matumizi ya kila siku ya nyumbani, lakini baba wa watu hakuwa na fedha kabisa.

Maskini wa Mungu, Mr. Chavek alipata tabu

kubwa sana. Aliendelea kuhangaika sana, maana alikuwa anadaiwa mkopo na benki na vilevile alikuwa anadaiwa na watu binafsi. Alishindwa hata kutoa kodi ya nyumba ya kuishi na akafukuzwa kwenye nyumba. Familia yake ilitabika sana. Maana hata hela ya kula haikuwepo.

Mr. Chavek alipata msongo wa mawazo, hali hiyo ilipelekea yeye kupooza mwili mzima.

Ndugu zake walijitahidi kumtibu ili waweze kunusuru uhai wake, lakini juhudi zao hazikuzaa matunda, Mr. Chavek aliaga dunia.

Je, tunajifunza nini kwa ndugu yetu Mr. Chavek na familia yake?

Tumeona madhara makubwa yaliyotokea kwa sababu ya usaliti wa Mr. Maliket kwa Mr. Chavek.

Madhara yaliyopatikana ni kama ifuatavyo;

Kwanza, familia ilimpoteza mpendwa wao kwa kutangulia mbele ya haki, na Mungu amrehemu apumzike kwa amani.

Pili, familia ilifukuzwa kwenye nyumba ya kupanga na ikaanza kutabika.

Tatu, watoto walipoteza ndoto zao za kimasomo.

Ona maumivu ambayo familia ilipitia kwa sababu ya usaliti!!

Inauma sana, sana, sana, sana!!

=====SEHEMU YA TATU======

Mbali na madhara yaliyopatikana kwenye familia na ndugu wa Mr. Chavek, watu wengi waliendelea kulia na kuomboleza kifo chake kwa muda mrefu.

Ilikuwa ni simanzi kubwa, giza lilitanda na hakuna aliyeamini kifo cha Mr. Chavek. Watu wengi walihisi wako ndotoni kumbe ni kweli Mr. Chavek alikuwa **amelala usingizi wa milele**. Watu walivuta kumbukumbu za aina ya uongozi wake kwenye kampuni. Alizingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali za uendeshaji wa makampuni.

Alikuwa ni mtu bora mwenye sifa za kipekee za uongozi.

Alikuwa kiongozi mtulivu na mvumilivu.

Hakuwahi kufanya maamuzi ya aina yoyote kwenye kampuni ya kuumiza au kunyanyasa mtu kwa sababu ya mihemuko ya watu.

Alikuwa ni kiongozi anayejiamini na kusimamia kitu alichokuwa anakiamini.

Aliweza kusikiliza ushauri kutoka kwa watu aliokuwa anawaongoza na kupokea miongozo mbalimbali kutoka kwa boss wake na taasisi mbalimbali zenye mamlaka hayo.

Mr. Chavek aliongoza kampuni kwa weledi mkubwa. Alikuwa mtu wa kutegemewa na wengi. Ukweli ni kwamba alikuwa mtu wa watu. Hakumuonea mtu yeyote katika mazingira ya kazi, kwake haki ya mtu ilikuwa kipaumbele.

Alimheshimu kila mtu bila kujali nafasi yake katika kampuni.

Alihakikisha anafanya mawasiliano mbalimbali kwa wafanyakazi wake. Maana aliamini mawasiliano yanaongeza ufanisi katika utendaji kazi kwenye kampuni.

Alikuwa na uwezo wa kubeba changamoto za wafanyakazi wake na kuzifanya kuwa changamoto zake. Ooh, katika hili, Mr. Chavek alikuwa mtetezi wa wanyonge kwani alikuwa na uwezo mkubwa wa kutatua changamoto za watu na kufanya maamuzi sahihi. Alipendwa na wafanyakazi na jamii iliyokuwainamzunguka.

Alijitahidi kuhakikisha anakuza ubunifu, uwajibikaji na fikra makini kazini, kwa wafanyakazi wake. Yaani, kwa kifupi alikuwa ni kiongozi wa kuonesha njia.

Aliacha alama kubwa sana kwenye kampuni kwa sababu ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha uongozi wake.

## ===SEHEMU YA NNE ====

Kreso, aliyekuwa mke wa marehemu Mr. Chavek, aliendelea kuteseka na watoto wake. Mama Chavek alipata pagale la nyumba na akaanza kuishi na watoto wake. Kipindi hicho hakuwa na hata fedha ya kukidhi mahitaji ya familia yake. Waliishi kwa kuwaomba wasamaria wema kusaidia familia. Mungu ni mwema, watu wachache walikuwa wanaguswa na jambo hilo na kutoa msaada kidogo kidogo. Kreso alianza kupambana na maisha angalau kupata fedha kidogo ya kuendesha maisha yake binafsi na familia yake.

Alianza kufanya biashara ndogo ndogo akawa anapata riziki kidogo kidogo. Yeye na watoto wake waliishi maisha ya kubana matumizi sana. Walikula mlo mmoja kwa siku ili angalau waweza kubakiza akiba ya kununua mahitaji mengine.

Mtoto wake mmoja aitwaye Dankris, aliyeacha chuo akiwa mwaka wa pili aliumia sana na namna walivyokuwa wakiishi maisha duni yaliyojaa ufukara wa hali ya juu. Akawa anamhoji mama yake, "Mama, tutaishi na maisha haya mpaka lini? Kwani

baba alifanya makosa gani kazini ambayo yanapelekea sisi kuishi maisha ya mateso namna hii? Mimi nataka nimfuate baba. Kreso, baada ya kusikia sentensi ya mwanae ya kutaka kumfuata baba, alishutuka na akamuuliza mwanaye, "Unasemaje?" Dankris akajibu: nataka nimfuate baba.

Kreso alilia kwa uchungu mkubwa sana. Wakati analia akaanza kusema, ooh, mume wangu, umeniachia majonzi makubwa na niko kwenye dimbwi la mawazo mithili ya bahari, tazama nilizoea ucheshi wako, uliishi kwa furahana wanao, familia ilifurahia uwepo wako nyumbani, ulijitahidi kutoa mahitaji ya familia yako, watoto walisoma bila tabu yoyote na ulisaidia ndugu zako, leo hii mimi ni mtu wa kuishi maisha haya! Ooh, Mungu nipe wepesi wa kukabili maisha haya ninayoishi. Tazama wanao wanavyoteseka. Mwanao Dankris anawaza kujiua. Mungu msalaba huu siwezi kuubeba.